TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# MODULI YA UJASIRIAMALI
# KIONGOZI CHA MWALIMU

TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA
ELIMU HAINA MWISHO

## HATUA YA PILI

IPOSA

TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# MPANGO WA ELIMU CHANGAMANI KWA VIJANA WALIO NJE YA SHULE

## KIONGOZI CHA MWALIMU
## MODULI YA UJASIRIAMALI

HATUA YA PILI

Kimeandaliwa na
Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
Dar es Salaam
**Tanzania, 2018**

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, 2018

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuchapa wala kurudufu kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

## DIBAJI

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI na UNICEF imeandaa Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (MECHAVI). Kwa lugha ya kingereza mpango huu unajulikana kama *"Integrated Programme for Out of School Adolscents - IPOSA.* Mpango huu umezingatia dhima ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya kutoa elimu bora kwa wote, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo ya Elimu. Katika kutekeleza program hii Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeandaa mtaala, mihutasari, moduli za masomo, miongozo ya kufundishia, upimaji na usimamizi kwa walimu wa MECHAVI. Kiongozi hiki kimeandaliwa kwa ajili ya mwalimu anayefundisha moduli ya Ujasiriamali hatua ya pili.

Kiongozi hiki kinamwelekeza mwalimu kufundisha kwa kusisitiza ujenzi wa umahiri na kutumia njia na mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji.

Ni matumaini yangu kuwa kwa kutumia kiongozi hiki walimu wataweza kutafsiri mtaala na muhtasari wa MECHAVI na kutumia moduli ipasavyo kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa ufanisi.

.......................................................

Dkt. Michael W. Ng'umbi

**Mkurugenzi Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

## SHUKURANI


Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) inapenda kutoa shukurani kwa wadau mbalimbali walioshiriki katika kufanikisha uandishi wa Kiongozi cha Mwalimu cha Moduli ya Ujasiriamali kwa vijana walio nje ya shule. Shukurani ziwaendee Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa kufadhili maandalizi ya programu hii pamoja na uandishi wa kiongozi hiki cha mwalimu. TEWW inaamini kuwa UNICEF na wadau wengine wa elimu wataendelea kufanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya kuwahudumia vijana wa Kitanzania wenye mahitaji anuwai kwa lengo la kuwainua kijamii na kiuchumi. Aidha, TEWW inathamini sana juhudi na mchango walioutoa katika kufanikisha kazi hii kwa manufaa ya watanzania.

Shukurani za pekee ziwaendee wataalamu wafuatao kwa juhudi zao za pamoja katika kukamilisha uandishi wa kiongozi hiki cha mwalimu:

**Waandishi:**

Baraka Kionywaki — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

Shemeli M. Magambo — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

**Mratibu:**

Dkt. Sempeho I. Siafu — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

**Mshauri:**

Dkt. Honest Kipasika — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

**Wachapaji:**

Zena Rajabu Kazala — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

Lovenes .S. Mrutu — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

..............................

Dkt. Naomi Katunzi

**Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

## YALIYOMO

DIBAJI .......... iii

SHUKURANI .......... iv

JINSI YA KUTUMIA KIONGOZI HIKI CHA MWALIMU .......... vi

SOMO LA KWANZA .......... 1

KUFAFANUA DHANA YA UJASIRIAMALI .......... 1

SOMO LA PILI .......... 6

KUANDAA MPANGO WA BIASHARA .......... 6

SOMO LA TATU .......... 12

KUFANYA BIASHARA KWA MAENDELEO .......... 12

REJEA .......... 23

## JINSI YA KUTUMIA KIONGOZI HIKI CHA MWALIMU

Kiongozi cha mwalimu kimeandaliwa ili kumsaidia mwalimu wa MECHAVI aweze kufundisha ipasavyo masomo yaliyopo katika moduli ya mwanafunzi HATUA YA PILI. Hatua hii ya pili ina lengo la kumpatia mwanafunzi umahiri wa ujasiriamali.

Muundo wa kiongozi hiki umejumuisha maeneo makuu matano. Maeneo hayo ni:

i) **Kusudi la somo**

ii) **Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

iii) **Njia na mbinu za uwezeshaji**

iv) **Hatua za somo**

v) **Tafakuri**

Ni muhimu kwa mwalimu kuelewa ipasavyo kila eneo ili aweze kufundisha na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

i) **Kusudi la Somo**

Eneo hili linamwelekeza mwalimu kufahamu malengo mahususi ambayo mwanafunzi anatakiwa kuyafikia mwishoni mwa somo.

ii) **Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Eneo hili linapendekeza baadhi ya vifaa ambavyo mwalimu anapaswa kuviandaa na kuvitumia wakati wa kufundisha. Hata hivyo mwalimu ana nafasi ya kuongeza vifaa vingine kadri anavyoona inafaa kulingana na mazingira halisi ya ujifunzaji.

iii) **Njia na mbinu za uwezeshaji**

Eneo hili limependekeza baadhi ya njia na mbinu ambazo mwalimu anapaswa kutumia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Njia hizo zinajumuisha majadiliano, mhadhara mfupi, maswali na majibu, bungua bongo, oneshombinu, mafunzo kwa vitendo, igizodhima, ziara za mafunzo na kualika mtaalamu. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu na

kutumia mbinu anuwai kulingana na mazingira ya darasa na wanafunzi.

**iv) Hatua za somo**

Hizi ni hatua zilizopendekezwa kufuatwa wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu unapaswa kufuata hatua hizi ili kufikia malengo kwa somo husika.

Hatua za somo pamoja na mbinu za kujifunzia zinategemea mambo mengine muhimu ikiwa ni pamoja na maandalizi mazuri ya mwalimu, idadi ya washiriki, sehemu ya kuendeshea mafunzo, muda pamoja na zana za kujifunzia na kufundishia.

**v) Tafakuri**

Katika eneo hili mwalimu unaelekezwa kuwaongoza wanafunzi wafanye tafakuri pamoja na mazoezi ili kupima uelewa kwa wanafunzi ~~juu ya~~ kuhusu somo husika. Tafakuri na mazoezi yafanyike mwishoni mwa somo na baada ya kukamilisha moduli.

### Nyenzo za Kuongoza Ujifunzaji

Ufundishaji unaojenga umahiri na unaomuweka mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji huzingatia mpango wa kujifunza wa mwanafunzi, tathmini binafsi ya mwanafunzi na tafakuri ya mwanafunzi kuhusu ujifunzaji wake. Hivyo basi unapaswa kuwaongoza wanafunzi kujiwekea malengo ya ujifunzaji, kutafakari na kujipima kuhusu ujifunzaji wao wenyewe. Fomu zifuatazo zimeandaliwa kukusaidia kuwaongoza wanafunzi kujiwekea malengo, kutafakari na kujipima ujifunzaji wao.

### Fomu ya Maendeleo Binafsi ya Mwanafunzi

Hii ni nyenzo muhimu kwa mwanafunzi kubainisha mambo ya kujifunza na kutilia maanani ujifunzaji wake ili kufikia umahiri aliokusudia. Nyenzo hii hutumika kama mpango kazi. Hatua za kuandika mpango wa maendeleo binafsi huongozwa na maswali yafuatayo:

- Nina umahiri kiasi gani kwa sasa kuhusu ujifunzaji wa somo hili?
- Ninakusudia kuweza kufanya nini kwa kujifunza somo hili?
- Nitachukua hatua gani ili niweze kufikia malengo yangu ya ujifunzaji?(mikakati ya ujifunzaji).

**Mfano wa Fomu ya Maendeleo Binafsi ya Mwanafunzi**

1. JINA....................... TAREHE.................

   Kabla ya kuanza somo eleza mambo yapi unayoweza kutenda kuhusu somo husika.

   - Ninaweza.......................................................

     .................................................................................

   - Nina mapungufu katika.......................................

     .................................................................................

2. Ungependa kuwa mahiri katika mambo yapi? ..........

   .................................................................................

   Malengo yangu ni yapi? ..........................................

   Ninataka kujifunza nini? ..........................................

   Nitajifunza kwa mikakati ipi?.........................................

3. Unapomaliza kujifunza somo husika tafadhali eleza:
   Je, nimefikia umahiri niliokusudia? ..........................

   .................................................................................

   .................................................................................

   .................................................................................

4. Je, ningependa kujifunza nini baada ya somo hili? Toa maelezo sahihi na hakikisha unakusudia umahiri unaoweza kuujenga. ..........................................

   .................................................................................

   .................................................................................

   .................................................................................

**ZINGATIA**

Fomu hizi zijazwe na kila mwanafunzi kila anapoanza kujifunza umahiri au somo husika. Lazima ziwasilishwe kwa mwalimu kila baada ya kujaza sehemu ya kwanza na ya pili. Baada ya kuhitimisha somo mwalimu huwarejeshea wanafunzi fomu zao ili wajaze sehemu ya tatu na ya nne na kuandaa mpango wa somo linalofuatia. Kwa kutumia fomu za maendeleo binafsi mwalimu anaweza kuboresha maandalizi yake ya ufundishaji kutokana na mahitaji yaliyobainishwa na wanafunzi.

### Fomu ya Tathmini ya Maendeleo ya Mwanafunzi

Fomu hii hujazwa baada ya mwanafunzi kumaliza kujifunza kwa vitendo. Hapa mwanafunzi anatathmini maendeleo yake mwenyewe kulingana na zoezi alilofanya. Nyezo hii inaweza kuwa na mpangilio ufuatao:

Moduli/ Kipindi.......................................

Zoezi alilopewa.......................................

1. Je unasemaje kuhusu utendaji wako? [weka alama ya (V)

   Hauridhishi

   Unaridhisha

2. Ni katika eneo gani unafikiri hujafanya vizuri?

   ..............................................................................

   ..............................................................................

   ..............................................................................

3. Utafanya nini kuimarisha utendaji wako?

   ..............................................................................

   ..............................................................................

   ..............................................................................

**Kumbuka**

> Nyenzo hii itamwezesha mwanafunzi ~~aweze~~ kupima maendeleo yake binafsi ya ujifunzaji. Waelekeze kuweka nyezo hii kwenye faili ambalo huitwa "mkoba wa kazi". Hivyo basi nyezo hii itakuwa sehemu ya mkoba wa kazi.

### Shajara ya Tafakuri

Fomu hii humwezesha mwanafunzi kufanya tafakuri kuhusu ujifunzaji wake. Kwa kufanya tafakuri, mwanafunzi huweza kuondokana na ufahamu wa mazoea na kujenga mtazamo mpya wa mambo yanayohusu somo alilojifunza. Aidha mwanafunzi huweza kujipambanua kwa fikra mpya tofauti na wenzake kutokana na ujifunzaji wa kina aliofanya.

### Tafakuri

Mwanafunzi anatafakari maendeleo yake mwenyewe ya ujifunzaji

### Mfano wa Shajara ya Tafakuri

Tafakuri ya Somo

1. Ni jambo gani lililokufurahisha zaidi katika somo hili?

   ..........................................................................

   ..........................................................................

   ..........................................................................

2. Utafanya nini ili uweze kutumia maarifa au stadi ulizojifunza kwa manufaa?

   ..........................................................................

   ..........................................................................

   ..........................................................................

3. Je, nini kifanyike ili uweze kujifunza vizuri zaidi kuhusu jambo hili?

.......................................................................................

.......................................................................................

.......................................................................................

**Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK)**

Eneo lingine ambalo limepewa umuhimu katika hatua hii ya pili ni kukazia stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu. Mwalimu unapaswa kwa kila somo uhakikishe unakazia stadi hizi. Hii itasaidia sana wanafunzi kumudu kwa ufasaha stadi za KKK.

Ni matarajio kuwa kiongozi hiki kitakusaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa hivyo unapaswa kukitumia ipasavyo.

# SOMO LA KWANZA
# KUFAFANUA DHANA YA UJASIRIAMALI

## Kipindi cha Kwanza

### Kusudi la somo

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana ya ujasiriamali na mjasiriamali
- Kubainisha sifa za mjasiriamali

1. **Vifaa vya Kufundishia na kujifunzia**

   Ubao, chaki, bangokitita, makapeni, moduli ya wanafunzi na vipeperushi

2. **Njia/mbinu za uwezeshaji**

   Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi na kualika mtaalam.

3. **Hatua za somo**

   **Hatua ya Kwanza**

   - Ongoza majadiliano kuhusu maana ya ujasiriamali na mjasiriamali kwa kuwaweka wanafunzi katika makundi madogo madogo ili waweze kujadili. Ili kusaidia majadiliano andaa maswali yafuatayo:

     a) Je, ulishawahi kusikia neno ujasiriamali?

     b) Katika eneo unalokaa ulishawaona watu wanafanya shughuli mbalimbali? Je, ni shughuli gani hizo?

     c) Je, shughuli zinazofanywa katika eneo lako zinaweza kuhusishwa na ujasiriamali?

     d) Je nini maana ya ujasiriamali?

     e) Nini tofauti kati ya ujasiriamali na Mjasiriamali?

- Zungukia kila kundi kutoa msaada panapohitajika.
- Watake kila kikundi wawasilishe majibu yao.
- Toa nafasi kwa wnafunzi waeleze maana ya ujasiriamali na Mjasiriamali.
- Mwalimu hitimisha kwa kueleza maana sahihi ya ujasiriamali na mjasiriamali pamoja na tofauti zake kisha waambie wanafunzi waandike katika daftari zao.

**Hatua ya Pili**

- Ongoza wanafunzi kusoma kifungu cha habari kuhusu ufanyaji biashara.
- Uliza maswali dadisi kuhusu ufanyaji biashara na ujasiriamali.
- Watake wanafunzi katika kila kundi wawasilishe kazi zao mbele ya darasa.

**Hatua ya Tatu**

- Gawa wanafunzi katika makundi madogo madogo.
- Ongoza wanafunzi katika makundi yao kusoma habari fupi kuhusu faida za mjasiriamali (angalia katika moduli ya mwanafunzi).
- Pitiakilakundinatoamsaadakwawalewatakaoshindwa kusoma kwa usahihi.
- Waongoze wanafunzi kuzitaja faida za kiuchumi na kijamii za mjasiriamali kutokana na kifungu cha habari walichosoma.
- Toa ufafanuzi wa majibu waliyoyatoa kisha toa faida za mjasiriamali za kiuchumi na kijamii kwa kuziandika ubaoni.
- Pitia wanafunzi kuhakikisha wanaandika kwa usahihi faida za mjasiriamali za kiuchumi na kijamii katika madaftari yao.

### Hatua ya Nne

- Ongoza majadiliano ya wanafunzi kuhusu sifa za mjasiriamali kwa kuuliza maswali dadisi.
- Fuatilia mjadala kwa kila kundi na toa msaada panapohitajika.
- Toa nafasi kwa kila kikundi kuweza kuwasilisha sifa za mjasiriamali walizo zijadili.
- Toa mhadhara mfupi kuhusu sifa za mjasiriamali ili wanafunzi wote wawe na uelewa wa pamoja. Mtake kila mwanafunzi aandike katika daftari lake sifa za mjasiriamali ~~kwenye daftari yake~~.
- Kagua daftari za wanafunzi ili uweze kutambua mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandika na mpe msaada kadri inavyowezekana.

### Hatua ya Tano

- Waongoze wanafunzi kujadili tofauti kati ya mjasiriamali na mfanyabiashara wa kawaida.
- Waambie wanafunzi wawasilishe majibu ya mjadala wao kuhusu tofauti kati ya Mjasiriamali na mfanyabiashara wa kawaida.
- Toa ufafanuzi kuhusu uwasilishaji wa wanafunzi kisha toa mhadhara mfupi kuhusu tofauti kati ya mfanyabiashara wa kawaida na Mjasiriamali ili wanafunzi wote wawe na uelewa wa pamoja.
- Watake wanafunzi waandike tofauti kati ya mjasiriamali na mfanyabiashara katika mkoba wa kazi.

## Kipindi cha Pili

### Kusudi la somo

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kubainisha vihatarishi vya ujasiriamali
- Kubainisha njia za kukabiliana na vihatarishi vya ujasiriamali

1. **Vifaa vya Kufundishia na kujifunzia**

   Ubao, chaki, makapeni, vipeperushi, vitini, video na moduli ya wanafunzi.

2. **Njia/mbinu za uwezeshaji**

   Majadiliano ya vikundi, simulizi, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi na kisa mafunzo.

3. **Hatua Za Somo**

**Hatua ya Kwanza**

- Toa mhadhara mfupi kuhusu changamoto zinazomkabili mjasiriamali katika shughuli zake za kujasiriamali.
- Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili changamoto za mjasiriamali.
- Toa mhadhara mfupi kwa kuandika ubaoni changamoto zinazomkabili mjasiriamali katika shughuli zake za kila siku ili wanafunzi wote wawe na uelewa wa pamoja.

**Hatua ya Pili**

- Wagawe wanafunzi katika makundi madogo madogo.
- Watake wanafunzi wajadili namna ya kukabiliana na vihatarishi vinavyomkabili mjasiriamali.
- Mwalimu pita katika kila kikundi kutoa msaada unaohitajika.
- Watake wanafunzi wawasilishe majibu ya mijadala yao.
- Toa mhadhara mfupi kisha andika ubaoni njia mbalimbali za kukabiliana na vihatarishi vinavyomkabili mjasiriamali.
- Watake wanafunzi waandike nukuu hizo katika daftari zao na watunze kwenye mikoba yao ya kazi.

**Hatua ya Tatu**

- Waongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari kilichopo katika moduli zao kinachohusu ujasiriamali na mjasiriamali.
- Pita kwa kila mwanafunzi kufuatilia usomaji wa habari hiyo ili kutoa msaada pale inapohitajika.
- Ongoza wanafunzi kutaja faida za mjasiriamali za kiuchumi na kijamii kwa kulinganisha na zile zilizopo katika moduli za wanakisomo.

**Hatua ya Nne**

- Waulize wanafunzi maswali yatakayosaidia kufanya tafakuri kuhusu mambo waliojifunza kuanzia hatua ya kwanza hadi ya tatu.
- Waelekeze wanafunzi ~~wafanye~~ wajibu maswali yaliyopo katika moduli zao kwenye kipengele cha zoezi.

## SOMO LA PILI

## KUANDAA MPANGO WA BIASHARA

**Kipindi cha Kwanza**

**Kusudi la somo**

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana ya biashara
- Kuainisha aina za biashara
- Kueleza maana na sifa za wazo la biashara

1. **Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

   Vipeperushi, vitabu, makapeni, bangokitita, moduli, ubao na chaki.

2. **Njia za uwezeshaji**

   Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo na mhadhara mfupi.

3. **Hatua za somo**

   **Hatua ya Kwanza**

   - Watake wanafunzi kueleza maana ya biashara
   - Andika ubaoni majibu ya wanafunzi
   - Waongoze kwenye jibu sahihi
   - Watake wanafunzi wataje aina za biashara
   - Wagawe wanafunzi katika makundi wajadili faida za kufanya biashara

   **Hatua ya Pili**

   - Waulize wanafunzi wazo la biashara maana yake nini
   - Waelekeze wanafunzi wasome kwenye moduli zao sifa za wazo zuri la biashara

**Hatua ya Tatu**

- Mwalimu toa mhadhara mfupi kuhusu maana ya biashara na aina zake ili wanafunzi wawe na uelewa wa pamoja.
- Toa mhadhara mfupi kuhusu maana na sifa za wazo zuri la biashara.
- Toa mhadhara mfupi kuhusu namna ya kutathmini na kuchagua wazo sahihi la biashara.

## Kipindi cha Pili

**Kusudi la somo**

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kueleza maaana ya mpango wa biashara.
- Kueleza sifa za mpango wa biashara.
- Kueleza hatua za uandaaji wa mpango wa biashara na umuhimu wa mpango huo.

**1. Vifaa vya uwezeshaji**

Vipeperushi, vitabu, makapeni, bangokitita, moduli, ubao na chaki.

**2. Njia za uwezeshaji**

Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi.

**3. Hatua za somo**

**Hatua ya Kwanza**

- Mwalimu watake wanafunzi waeleze maana ya mpango wa biashara.
- Waongoze wanafunzi kutaja sifa za mpango wa biashara.

#### Hatua ya Pili

- *Waongoze wanafunzi kusoma kwenye moduli zao* hatua za uandaji wa mpango wa biashara.
- Wagawe wanafunzi katika vikundi wajadili umuhimu wa kuanda mpango wa biashara.

#### Hatua ya Tatu

- Waongoze wanafunzi wataje changamoto katika uandaaji wa mpango wa biashara.
- Waongoze wanafunzi wajadili namna ya kutatua changamoto katika uandaaji wa mpango wa biashara.
- Toa mhadhara mfupi kuhusu namna ya kutatua changamoto katika uandaaji wa mpango wa biashara ili wanafunzi wawe na uelewa wa pamoja.

## Kipindi cha Tatu

### Kusudi la somo

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kueleza vipengele vya mpango wa biashara.
- Kusoma habari fupi kuhusu mpango wa biashara.

1. **Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

   Vipeperushi, vitabu, makapeni, bangokitita, moduli, ubao na chaki.

2. **Njia/mbinu za uwezeshaji**

   Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi.

3. **Hatua za somo**

   **Hatua ya Kwanza**

   - Waongoze wanafunzi kutaja vipengele vya mpango wa biashara vilivyoandikwa kwenye moduli zao.
   - Toa mhadhara mfupi kufafanua kila kipengele cha mpango wa biashara.

**Hatua ya Pili**

- Mwalimu waongoze wanafunzi kusoma habari fupi kuhusu mpango wa biashara (angalia katika moduli ya mwanafunzi).
- Wape wanafunzi muda wa kutafakari habari fupi ya mpango wa biashara waliosoma kwenye moduli zao.

**Hatua ya Tatu**

- Waongoze wanafunzi kila mmoja aweze kuandika habari fupi kuhusu kuandaa mpango wa biashara.
- Toa mhadhara mfupi ukifafanua kwa kuandika ubaoni tofauti ya faida ghafi na faida halisi.
- Toa mhadhara mfupi kufafanua zaidi umuhimu wa mpango wa biashara.

## Kipindi cha Nne

**Kusudi la somo**

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kubaini vyanzo vya fedha na mtaji wa biashara,
- Kuandika habari fupi kuhusu mpango wa biashara

**1. Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

Vipeperushi, vitabu, makapeni, bangokitita, moduli, ubao na chaki

**2. Njia/mbinu za uwezeshaji**

Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi, kualika mtaalamu

**3. Hatua za somo**

**Hatua ya Kwanza**

- Waulize wanafunzi maana ya mtaji wa biashara.
- Waongoze wanafunzi kubainisha vyanzo vya fedha vya mtaji wa biashara.

**Hatua ya Pili**

- Alika mtaalam wa fedha atoe mhadhara mfupi kuhusu namna ya kupata fedha kutoka kwenye taasisi za kifedha kwa ajili ya kufanyia biashara.
- Wagawe wanafunzi katika vikundi wajadili changamoto za upatikanaji wa mtaji wa biashara.
- Fuatilia mjadala wa kila kundi ili ubaini mapungufu ya wanafunzi na toa msaada panapohitajika.

**Hatua ya Tatu:**

Mwalimu waongoze wanafunzi kuandika habari fupi kuhusu mpango wa biashara bila kunakili kwenye moduli zao.

## Kipindi cha Tano

**Kusudi la somo**

Kumfundisha mwanafunzi ili aweze:

Kutumia matendo ya hesabu katika kuandaa mpango wa biashara.

1. **Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

   Vipeperushi, vitabu, makapeni, bangokitita, moduli, ubao na chaki.

2. **Njia/mbinu za uwezeshaji**

   Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi, kualika mtaalamu.

3. **Hatua za somo**

   **Hatua ya Kwanza**

   - Waongoze wanafunzi kuandika mpango wa biashara kwa kufuata vipengele vyote.
   - Toa mhadhara mfupi namna ya kupanga bei na kukokotoa faida.

**Hatua ya Pili**

- Fanya majumuisho ya mada yote kwa kuwauliza wanafunzi jambo waliloelewa kwa ufasaha na lipi hawakuelewa kwa ufasaha.
- Wape wanafunzi maswali yaliyoandikwa kwenye moduli wajibu kwenye daftari zao ili uweze kutathmini uelewa wao.

# SOMO LA TATU

## KUFANYA BIASHARA KWA MAENDELEO

### Kipindi cha Kwanza

**Kusudi la somo**

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana ya kusajili biashara
- Kueleza umuhimu wa kusajili biashara
- Kueleza hatua za kusajili biashara

1. **Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

   Moduli ya wanafunzi, vitini, makapeni, ubao, chaki, bunguabongo, vipeperushi, bangokitita, vipeperushi.

2. **Njia/mbinu za uwezeshaji**

   Mhadhara mfupi, majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo na kualika mtaalam

3. **Hatua za somo**

   **Hatua ya Kwanza**

   - Panga wanafunzi katika vikundi vidogovidogo ili wajadili maana ya kusajili biashara kwa kuwapatia maswali dadisi yafuatayo:
     a) Je ulishasikia neno biashara iliyosajiliwa?
     b) Nini maana ya kusajili biashara?
     c) Kuna maufaa gani yanayopatikana kwa kusajili biashara?
   - Pita kwa kikundi kimoja kimoja ili kutoa msaada pale inapobidi.
   - Waongoze wanafunzi kwa kila kikundi kuwasilisha majibu yao mbele ya darasa.

- Toa mhadhara mfupi kuhusu maana ya kusajili biashara kisha sahihisha majibu ya kila kikundi kwa ujumla na andika maana ya kusajili biashara ubaoni.
- Ongoza wanafunzi kuandika maana ya kusajili biashara katika madaftari yao.
- Pita kwa wanafunzi ili kusahihisha makosa ya uandikaji.

**Hatua ya Pili**

- Wapange wanafunzi katika makundi madogomadogo kisha wapatie maswali dadisi ili wajadiliane umuhimu wa kusajili biashara.
- Ongoza majadiliano kuhusu umuhimu wa kusajili biashara kwa kuwazungukia wanafunzi katika vikundi vyao kutoa msaada pale panapohitajika.
- Waongoze wanafunzi kuwasilisha kazi zao.
- Waelekeze wanafunzi walinganishe majibu yao na yale yaliyopo katika moduli.

**Hatua ya Tatu**

- Waambie wanafunzi wajadili katika makundi yao hatua za kusajili biashara.
- Pita kwa kila kundi ili kujiridhisha kama wanafunzi wanajadili hatua za kusajili biashara.
- Watake wanafunzi wa kila kundi wawasilishe majibu ya mjadala wao.
- Toa mhadhara mfupi kuhusu hatua za kusajili biashara ili wanafunzi wote wawe na uelewa wa pamoja.
- Mwalimu andika hatua zote za kusajili biashara katika bangokitita.
- Mwalimu mtake kila mwanafunzi aandike kwenye daftari yake/ubao

### Kipindi cha Pili

**Kusudi la somo**

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana na aina za soko.
- Kueleza maana ya masoko.
- Kueleza mambo muhimu katika masoko (B4).

**1. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Moduli ya wanafunzi, vitini, makapeni, ubao, chaki, vipeperushi, bangokitita, vipeperushi.

**2. Njia/mbinu za uwezeshaji**

Mhadhara mfupi, majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo na kualika mtaalam.

**3. Hatua za somo**

**Hatua ya Kwanza**

- Waongoze wanafunzi kuunda vikundi ili kujadili maana na aina za soko kwa kuwapatia maswali dadisi yafuatayo:
  a) Wapi unaponunua bidhaa zako za kila siku?
  b) Nini maana ya soko?
  c) Sifa za soko ni zipi?
- Fuatilia mjadala wa kila kundi ili kutoa msaada pale inapohitajika.
- Watake wanafunzi wawasilishe kazi zao mbele ya darasa.
- Toa mhadhara mfupi kufafanua maana na aina za soko kwa kuandika katika bangokitita.
- Watake wanafunzi waandike maana na aina za soko katika daftari zao

**Hatua ya Pili**

- Wagawe wanafunzi katika makundi.
- Waongoze wanafunzi katika makundi yao kusoma habari fupi kuhusu maana ya masoko ( angalia moduli ya mwanafunzi).
- Wapitie wanafunzi katika makundi yao ili kutoa msaada pale panapohitajika.
- Waelekeze wanafunzi kuwasilisha kazi zao.
- Linganisha majibu yao na yale yaliyopo katika moduli zao, yasahihishe kisha watake waandike katika madaftari yao.

**Hatua ya Tatu**

- Waambie wanafunzi wajadili nguzo nne (B4) muhimu za masoko.
- Pita katika kila kundi ili uweze kujua kama wanafunzi wanaweza kubaini nguzo nne muhimu za masoko.
- Waelekeze wanafunzi kuwasilisha kazi zao.
- Toa mhadhara mfupi kuhusu nguzo nne muhimu za masoko (B4).

**Hatua ya Nne**

Waulize wanafunzi maswali yatakayosaidia kutafakari mambo waliojifunza kuanzia hatua ya kwanza hadi ya tatu.

## Kipindi cha Tatu

**Kusudi la somo**

Kumfundisha mwanafunzi ili aweze:

- Kueleza maana ya biashara ya familia.
- Kubaini uhusiano kati ya biashara na taasisi.
- Kueleza maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara.
- Aina na njia za kutunza kumbukumbu za biashara.

1. **Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

   Ubao, chaki, bangokitita, makapeni, moduli ya wanafunzi, vitini na vipeperushi.

2. **Njia/mbinu za uwezeshaji:**

   Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi, kisa mkasa, ziara mafunzo na kualika mtaalam.

3. **Hatua za somo**

   **Hatua ya Kwanza**

   - Ongoza majadiliano kuhusu maana ya biashara ya familia na mazingira yake.
   - Uliza maswali dadisi kuhusu maana ya biashara ya familia na mazingira yake.
   - Pita katika kila kundi kutoa msaada inapobidi.
   - Watake wanafunzi katika kila kundi wawasilishe majibu ya kazi yao.
   - Toa nafasi kwa kila kundi waeleze maana ya biashara ya familia na mazingira yake.
   - Toa maana sahihi ya biashara ya familia na mazingira yake kisha watake wanafunzi waandike katika daftari zao.

   **Hatua ya Pili**

   - Waongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari kuhusu uhusiano wa biashara na taasisi
   - Uliza maswali dadisi kuhusu uhusiano kati ya biashara na taasisi
   - Watake wanafunzi wajadili uhusiano kati ya biashara na taasisi
   - Watake wanafunzi wawasilishe kazi zao mbele ya darasa.
   - Fanya masahihisho pale walipokosea.
   - Toa mhadhara mfupi kufafanua zaidi uhusiano kati ya biashara na taasisi.

### Hatua ya Tatu

- Waongoze wanafunzi katika makundi yao kusoma habari fupi kuhusu maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara (angalia katika kitabu cha mwanafunzi).
- Pitia makundi ya wanafunzi na kutoa msaada kwa wale watakaoshindwa kusoma kwa usahihi.
- Waongoze wanafunzi kueleza maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara kutokana na kifungu cha habari walichosoma.
- Toa ufafanuzi wa majibu waliyoyatoa kisha toa mhadhara mfupi ukieleza maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara kwa kuziandika ubaoni.
- Watake wanafunzi wote waandike kwa usahihi maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara katika madaftari yao.

### Hatua ya Nne

- Wagawe wanafunzi katika vikundi vidogovidogo ili kujadili ~~kuhusu~~ aina na njia za kutunza kumbukumbu za biashara.
- Watake wanafunzi wajadili katika makundi yao aina na njia za kutunza kumbukumbu za biashara.
- Pitia kila kundi kufuatilia mjadala wa njia za kutunza kumbukumbu za biashara.
- Watake wanafunzi katika kila kundi wawasilishe matokeo ya mjadala wao.
- Toa nafasi kwa kila kikundi ~~kuweza~~ kuwasilisha matokeo ya mjadala wao.
- Toa mhadhara mfupi kuhusu aina na njia za kutunza kumbukumbu za biashara.
- Watake wanafunzi wote waandike katika daftari zao.

## Kipindi cha Tano

### Kusudi la somo

Kumfundisha mwanafunzi aweze

- Kukokotoa gharama
- Kupanga bei
- Kukokotoa faida na hasara

1. **Vifaa vya Kufundishia na kujifunzia**

   Ubao, chaki, bangokitita, makapeni, moduli ya wanafunzi, vitini na vipeperushi

2. **Njia/mbinu za uwezeshaji:**

   Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi, kisa mkasa, ziara mafunzo na kualika mtaalam.

3. **Hatua za somo**

   **Hatua ya Kwanza**

   - Waulize wanafunzi nini maana ya gharama za biashara
   - Watake wanafunzi kutaja bayana aina ya gharama za biashara
   - Wagawe wanafunzi katika makundi wajadili kuhusu ukokotoaji wa gharama ya biashara
   - Pita katika kila kundi uone wanafunzi wanajadili na toa msaada panapohitajika
   - Watake wanafunzi kwa kila kikundi wawasilishe matokeo ya majadiliano yao
   - Toa mhadhara mfupi kuhusu ukokotoaji sahihi wa gharama za biashara kisha watake wanafunzi wote waandike katika daftari

   **Hatua ya Pili**

   - Waulize wanafunzi maana ya bei
   - Waambie wanafunzi katika makundi wajadili namna ya kupanga bei

- Waelekeze wanafunzi kuwasilisha kazi zao.
- Toa ufafanuzi kuhusu uwasilishaji wa wanafunzi kisha toa mhadhara mfupi kuelekeza wanafunzi namna ya kupanga bei kwa kuandika katika bango kitita.
- Waambie wanafunzi waandike katika daftari zao.

**Hatua ya Tatu**

- Wagawe wanafunzi katika vikundi vidogovidogo.
- Waongoze wanafunzi katika makundi yao kusoma habari fupi kuhusu maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara (angalia katika kitabu cha mwanafunzi).
- Pitia makundi ya wanafunzi na kutoa msaada kwa wale watakaoshindwa kusoma kwa usahihi.
- Waongoze wanafunzi kueleza maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara kutokana na kifungu cha habari walichosoma.
- Toa ufafanuzi wa majibu waliyoyatoa kisha toa maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara kwa kuziandika ubaoni.
- Pitia wanafunzi katika kila kundi kuhakikisha wanaandika kwa usahihi maana na umuhimu wa kumbukumbu za biashara katika madaftari yao.

**Hatua ya Nne**

- Wagawe wanafunzi katika vikundi vidogovidogo ili kujadili maswali kuhusu kukokotoa faida na hasara.
- Ongoza majadiliano kuhusu ukokotoaji wa faida na hasara kwa kuwapatia maswali ya mfano.
- Pitia makundi yote kufuatilia mjadala wa ukokotoaji wa faida na hasara.
- Toa nafasi kwa kila kikundi kuweza kuwasilisha kukokotoa faida na hasara.
- Kokotoa swali la mfano lililopo katika vitabu vya wanafunzi kuhusu faida na hasara.
- Waambie wanafunzi waandike katika daftari zao.

**Kipindi cha ~~Sita~~**

**Kusudi la somo**

Kumfundisha mwanafunzi aweze:

- Kueleza dhana na maana ya vikundi vya ujasiriamali
- Kueleza aina na umuhimu wa vikundi vya ujasiriamali
- Mbinu za kuanzisha vikundi vya ujasiriamali
- Mbinu za kuendeleza vikundi vya ujasiriamali

1. **Vifaa vya Kufundishia na kujifunzia**

   Ubao, chaki, bangokitita, makapeni, moduli ya wanafunzi, vitini na vipeperushi

2. **Njia/mbinu za uwezeshaji:**

   Majadiliano, maswali na majibu, bunguabongo, mhadhara mfupi, kisamafunzo, ziara mafunzo

3. **Hatua za somo**

   **Hatua ya Kwanza**

   - Waambie wanafunzi wajadili kuhusu dhana na maana ya vikundi vya ujasiriamali
   - Waulize wanafunzi maswali dadisi kuhusu dhana na maana ya vikundi vya ujasiriamali
   - Pita katika kila kundi kutoa msaada inapobidi
   - Watake wanafunzi kwa kila kundi wawasilishe majibu yao
   - Toa mhadhara mfupi kuhusu dhana na maana ya vikundi vya ujasiriamali kwa kuandika katika bangokitita ili wanafunzi wote wawe na uelewa wa pamoja
   - Waambie wanafunzi waandike kwenye daftari zao na watunze katika mikoba yao ya kazi

**Hatua ya Pili**

- Wagawe wanafunzi katika makundi madogomadogo wajadili aina na umuhimu wa vikundi vya ujasiriamali

- Watake wanafunzi katika kila kundi wawasilishe kazi zao mbele ya darasa.
- Toa ufafanuzi kuhusu uwasilishaji wa wanafunzi kisha elekeza aina na umuhimu wa vikundi vya ujasiriamali kwa kuandika katika bango kitita.

**Hatua ya Tatu**

- Wagawe wanafunzi katika vikundi vidogovidogo.
- Waongoze wanafunzi katika makundi yao kusoma habari fupi kuhusu mbinu za kuanzisha vikundi vya ujasiriamali (angalia katika moduli ya mwanafunzi).
- Pitia makundi ya wanafunzi na kutoa msaada kwa wale watakaoshindwa kusoma kwa usahihi.
- Waongoze wanafunzi kueleza mbinu za kuanzisha vikundi vya ujasiriamali kutokana na kifungu cha habari walichosoma.
- Toa ufafanuzi wa majibu waliyoyatoa kisha toa mbinu sahihi za kuanzisha vikundi vya ujasiriamali kwa kuziandika ubaoni.
- Pitia wanafunzi kuhakikisha wanaandika kwa usahihi mbinu za kuanzisha vikundi vya ujasiriamali katika madaftari yao.

**Hatua ya Nne**

- Waambie wanafunzi wajadili mbinu za kuendeleza vikundi vya ujasiriamali.
- Ongoza majadiliano kuhusu mbinu za kuendeleza vikundi vya ujasiriamali.
- Pitia katika kila kikundi kufuatilia mjadala wa mbinu za kuendeleza vikundi vya ujasiriamali na toa msaada panapohitajika.
- Toa nafasi kwa kila kikundi kuweza kuwasilisha majibu yao
- Toa mhadhara mfupi kuhusu mbinu za kuendeleza vikundi vya ujasiriamali ili wanafunzi wote wawe na uelewa wa pamoja.

**Hatua ya Tano**

- Waulize wanafunzi maswali yatakayosaidia kutafakuri mambo waliojifunza kuanzia hatua ya kwanza hadi ya nne.
- Waelekeze wanafunzi wafanye maswali yaliyopo katika moduli zao kwenye kipengele cha zoezi.

Kipindi cha pili

- Kusoma -

## REJEA

Kiyosaki, R. and Lechter, S. (2002) Rich Dad, Poor Dad. Tangtan. Network

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (2017) *Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Nje ya Shule*. Dar es Salaam

UNICEF (2003) *Elimu Rika na Stadi za Maisha*: Mwongozo wa Wawezeshaji. Dar es Salaam

**Printed By:** Institute of Adult Education
S.L.P 20679, Dar es Salaam, Tanzania
Tel:+255 22 2150838, Fax: +255 22 2150836
Website:www.iae.tz Email:info@iae.ac.tz